

MTIHANI WA TATHMINI-WILAYA YA NANDI MASHARIKI 2009

102/3

KISWAHILI

**KARATASI YA TATU
JULAI/AGOSTI, 2009**

MUDA: SAA: 2 ½

SWALI LA 1: UTENGANO –S.A MOHAMED:

1. “Mimi nilidhani umepata motto mwenye sura na tabia zake, motto mwenye kwao-nimesafiri kwa mweno wa meli mia mbili na hamsini na hamsini kujanileta kwa mtu asiye na asili wala fasili?”
 - (a) eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)
 - (b) Kwa nini mzungumiwa anasema kuwa hana asili wala fasili. (alama 10)
 - (c) Amesafiri kuja kuja kufanya nini/ (alama 2)
 - (d) Taja mbinu za lugha zilizotumika kwenye dondoo hili na umuhimu wake. (alama 4)

2. **TAMTHILIA:**
KITHAKA WA MBERIA-KIFO KISIMANI:
“ kauni za Butangi zinapovunjwa ili kuridhisha maraafiki zake, uko radhi kuyafumba macho ili yasione kinachoendelea.”
 - (a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)
 - (b) eleza wasifu wa mzungumzaji kwa kurejelea tamthilia nzima. (alama 8)
 - (c) Taja na ueleza maudhui yanayodokezwa na kauli hii. (alama 8)

3. Ukitoa ithibati kwenye Tamthilia ya Kifo Kisimani, eleza sifa na umuhimu wa mhusika Mwelusi. (alama 20)

**MAYAI WAZIRI WA MARADHI:
CLARA MOMANGI: NGOME YA NAFSI:**

“Haidhuru mutate,bea. Ni heri kuliwa na mnyama mwitu kuliko kufungiwa ndani ya ngome.”

- (a) Kwa mjibu w hadithi hii, fafania maana ya ngome. (alama 2)
- (b) Mzungumzaji alikumbana na matatizo yapi katika maisha yake? (alama 8)
- (c) Kwa nini mzungumzaji alikata ngome aliyokusudiwa kuingia? (alama 5)
- (d) Taja mbinu mbili zinazojitokeza katika dondoo hili (alama 2)
- (e) Ni haki zipi tatu za watoto zilizokiukwa katika hadithi hii ? (alama 3)

FUMBO LA MWANA- SINJIRI MUKUBA;

5. Eleza sifa na tabia za wahusika wafuatao wa hadithi hii ya Fumbo la Mwana. (alama 20)

- (i) Mzee Atanasi Mukasa.
- (ii) Nanda.
- (iii) Makulu
- (iv) Mwalimu Mkuu.

6. (a) (i) Fafania maana ya methali. (alama 2)
(ii) Fafania sifa tano za methali. (alama 5)
- (b) (i) Ngomezi ni sanaa ya aina gain? (alama 1)
(ii) Bainisha sifa za ngomezi. (alama 4)
- (c) (i) Eleza jinsi fasihi simulizi inavyohitaji siku hizi (alama 4)
(ii) Taja nne za kukusanya Fasihi Simulizi. (alama 4)

6. SEHEMU YA C: USHAIRI

Soma shairi lifuatalo kasha uyajibu maswali:

WANANAMBIA MCHAFU (Na Said A. A. Mohamed)

1. Wananambia, naharibu utu wangu,
Wananambia, nalizika jina langu,
Wananambia, na kutaja siri zangu,
Bali wanashindwa kuchungua kisa changu.
2. Wananisubi, machafu matendo yangu,
Wananisubu, najivua nguo,
Wananisubu, siujali uke wangu,
Bali wanashindwa kuchungua kisa changu.
3. Wanahujumu, asili ya damu yangu,
wanhujumu, tonge na kivazi changu,
Wanahujumu, nyendo na shughuli zangu,
Bali wanashindwa kuchungua kisa changu.

4. Wananilani, baba hata mama yangu,
wananilani, wasema sisifu Mungu,
Hawatafuti, tamu na wangu uncungu,
Bali wanashindwa, kuchungua kisa changu.
5. Hawatafuti, wakajua shida zangu,
Hawatafuti, kisa cha uchafu wangu
Hawatafuti , tamu na wangu uchugu.
Bali wanashindwa, kuchungua kisa changu.
6. Nawauliza, nani apendaye pingu?
Nawauliza, machafu ya ulimwengu,
Nawauliza, nielezeni wenzangu,
Bali wanashindwa kuchungua kisa changu.
7. Nawaelezea, nimemaliza mizungu,
Nawaelezea, uchafu si haja yangu,
Nawaelezea, nawapeni siri yangu,
Bali wanashindwa kuchunguza kisa changu.

Maswali;

- (a) Taja na ueleze kwa kutolea mifano bahari ziliztumika katika shairi hili, (alama 3)
- (b) Fafanua umbo la shairi hili. (alama 3)
- (c) (i) Mtunzi/mlalamishi katika shairi hili ni nani? (alama 1)
- (ii) Thibitisha (alama 1)
- (d) Mtunzi anaonyesha kurerwa na mambo mbalimbali, yaeleze. (alama 4)
- (e) andika ubeti wa sita kwa lugha nathari. (alama 4)
- (f) Fafanua maneno yafuatayo kwa mujibu wa shairi. (alama 4)
- (i) Wananisubu
- (ii) Mizungu.
- (iii) Wanahujumu
- (iv) Wanahujumu
- (v) Nyendo.